**HOTUBA YA IJUMAA**

**Kupambana na uharibifu ni jukumu la kidini kitafaifa na kijamii**.

Imefasiriwa na

Profesa.Ayman Al-asar

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, mwenye kusema ndani ya Kitabu chake: **وَلا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ لا يُحِبُّ الْمُفْسِدِين** {**Wala usitafute kufanya uharibifu katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wahaibifu**}, ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki ispokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad S.A.W ni Mtume wake na Mja wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake Mtume pamoja na watu nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale waliomfuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi huo:**

Ufisadi na uharibifu kwa ujumla ni tukio mbaya lenye kuharibu na kubomoa nguvu za watu na nchi kwa ujumla, na kuwa ni kikwazo kwenye ujenzi na maendeleo, hivyo zimekuja Sharia za mbinguni zikikubaliana na tahadhari ya uharibifu kwa sura zake na namna zake zote, ambapo Anasema Mola Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Saleh A.S: **"وَلَا تَعْثَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ"** {**Wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu**} na Anasema tena Mola Mtukufu:

**وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْثَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ.**

{**wala msiwahini watu vitu vyao; wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu**}. Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Musa A.S akiwa anamwambia ndugu yake Haruna A.S: **وَأَصْلِحْ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ** {**Na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu**}. Na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W:

**فَأَمَّا مَن ابْتَغَى وَجْهَ اللَّهِ، وَأَطَاعَ الْإِمَامَ، وَأَنْفقَ الْكَرِيمَةَ، وَيَاسَرَ الشَّرِيكَ، وَاجْتَنَبَ الْفَسَادَ، فَإِنَّ نَوْمَهُ وَنُبْهَهُ أَجْرٌ كُلُّه**

**"***Ama mwenye kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na akamtii kiongozi, akatoa kwa ridhaa ya nafsi yake, akamfanyia upole na wepesi mwenzake na akajitenga na vitendo vya uharibifu basi usingizi wake na kuamka kwake vyote ni malipo kwake*".

Uharibifu una sura nyingi, hatari zaidi ni inayohusiana na ukiukaji wa mali na utawala kupitia vitendo vya uharibifu wa mali ya umma, na kuzembea katika kutekeleza wajibu wa kikazi ikiwa na kujihusisha na vitendo vya rushwa na udanganyifu, yote haya ni katika mlango wa kula haramu na kula mali za watu kwa njia batili, ambapo Anasema Mola Mtukufu: **وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ** {**Wala msiliane mali zenu kwa njia batili**}. Na Anasema Mtume Muhammad S.A.W:

**لعنةُ اللهِ على الرّاشِي والمُرْتَشِي**

**"***Mwenyezi Mungu amemlaani mtoa rushwa na mpokea rushwa*" na anasema tena Mtume S.A.W: **إِنَّ رِجَالًا يَتَخَوَّضُونَ فِي مَالِ اللَّهِ بِغَيْرِ حَقٍّ ، فَلَهُمُ النَّارُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ** "*Hakika watu wanaojipatia mali za Mwenyezi Mungu bila ya haki basi wana adhabu ya moto siku ya kiyama*". Na anasema Mtume S.A.W: **لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ لَحْمٌ نَبَتَ مِنْ سُحْتٍ، النَّارُ أَوْلَى بِه**

"*Hatoingia Peponi mtu ambaye mwili wake umeimarika kutokana na chakula haramu kwani moto ni bora kwake*". Na anasema tena Mtume S.A.W:

**مَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا.**

"*Mwenye kufanya udanganyifu wa kughushi vitu basi huyo si katika sisi*".

Katika mambo yasiyokuwa na shaka yeyote ndani yake ni kuwa kupambana na uharibifu kunachukuliwa ni jukumu la kidini kitaifa na kijamii, kwani jukumu la

kidini linaanzia kwenye marekebisho ya nafsi na kuilea kwenye misingi ya kumcha-Mungu na uangalizi wake wa siri na wazi, ambapo anasema Mola Mtukufu:

**وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ.**

{**Yeye yupo pamoja na nyinyi popote mutakapo kuwepo na Mwenyezi Mungu kwa yale muyafanyanyo ni Mwenye kuyaona**}.

Na Anasema tena Mola Mtukufu: **إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا** {**Hakika Mwenyezi Mungu ni muangalizi kwenu**}, kama vile inawajibika kupandikiza misingi ya ukweli uaminifu utekelezaji na mengine katika misingi bora kwenye nafsi, kwani Waumini wa kweli ni wa jenzi na wala si waharibifu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**أَمْ نَجْعَل الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَم نَجْعَل الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ.**

{**Je! Tuwafanye walio amini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au tuwafanye wacha-Mungu kama waovu?**}.

Ama jukumu la kitaifa linahitaji kuimarisha misingi ya uzalendo na kuimarisha hisia za kuona jukumu lipo kwenye mali za uma na maeneo ya uma, pia kueneza utamaduni wa uwazi katika wigo mpana na wa jamii, na kuwazuia mafisadi na wabomoaji, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaahidi waharibifu duniani kuwaadhibu adhabu kali ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَن يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُم مِّنْ خِلَافٍ أَوْ يُنفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ذَٰلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ.**

{**Basi malipo ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusulubiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchini. Hii ndiyo adhabu yao katika dunia; na Akhera watapata adhabu kubwa**}.

**HOTUBA YA PILI.**

Shukrani ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehema na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume wetu Muhammad SAW pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakika jukumu la kijamii linahitaji kuimarisha utamaduni wa uma unaopinga uharibifu na kufikia usimamizi wa kijamii wenye kufahamu hatari ya uharibifu kwa jamii nzima, na hilo ni kupitia kuboresha nafasi ya taasisi za kidini kielemu na kihabari, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**فَلَوْلاَ كَانَ مِنَ الْقُرُونِ مِن قَبْلِكُمْ أُوْلُواْ بَقِيَّةٍ يَنْهَوْنَ عَنِ الْفَسَادِ فِي الأَرْضِ إِلاَّ قَلِيلاً مِّمَّنْ أَنجَيْنَا مِنْهُمْ**

{**Basi mbona hawa kuwamo katika watu wa kabla yenu wenye vyeo na wasaa wanao kataza uharibifu katika nchi, isipo kuwa wachache tu, ambao ndio tulio waokoa**}.

Na anasema tena Mola Mtukufu: **وَمَا كَانَ رَبُّكَ لِيُهْلِكَ الْقُرَى بِظُلْمٍ وَأَهْلُهَا مُصْلِحُونَ**

{**Wala hakuwa Mola wako Mlezi wa kuihilikisha miji kwa dhuluma tu na hali watu wake ni watenda mema**}.

Kama vile jambo lenyewe linahitaji kuto mficha muharibifu yeyote, bali kutoa ushirikiano na vyombo vya usalama ili hali ya utulivu iendelee kuenea kwenye jamii nzima, ambapo anasema Mtume Muhammad SAW:

**مَثَلُا لْقَائِمِ عَلَى حُدُودِ اللَّهِ وَالْوَاقِعِ فِيهَا كَمَثَلِ قَوْمٍ اسْتَهَمُواعَلَى سَفِينَةٍ فَأَصَابَ بعْضُهُمْ أَعْلَاهَا وَبَعْضُهُمْ أَسْفَلَهَا فَكَانَ الَّذِينَ فِي أَسْفَلِهَا إِذَا اسْتَقَوْامِنْ الْمَاءِ مَرُّواعَلَى مَنْ فَوْقَهُمْ فَقَالُوا لَوْأَنَّا خَرَقْنَا فِي نَصِيبِنَا خَرْقً اوَلَم نُؤْذِ مَنْ فَوْقَنَا فَإِنْ يَتْرُكُوهُمْ وَمَاأَرَادُوا هَلَكُواجَمِيعًا وَإِنْ أَخَذُوا عَلَى أَيْدِيهِم نَجَوْاوَنَجَوْاجَمِيعًا.**

“Mfano wa wenye kusimamia mipaka ya Mwenyezi Mungu na wale wenye kukiuka mipaka hiyo ni sawa na watu waliopanda jahazi moja baadhi yao wapo sehemu ya juu ya jahazi na wengine wakiwa sehemu ya chini, wakawa wale waliokaa chini pindi wanapotaka maji wanalazimika kwenda kwa walio juu yao kisha wakasema, kama tutatoboa sehemu ili tupate maji hatutawafanyia kero wale walio juu yetu, hivyo wakiwa wataachwa na jambo lao hilo wanalotaka

kulifanya basi wataangamia wao wote na ikiwa watazuiwa kufanya hivyo basi wataokoka na kuokoa wote.

**Ewe Mwenyezi Mungu ihifadhi Misri na kila aina ya ubaya pamoja na nchi zengine za Kiarabu na Kiislamu.**